



MKATABA WA KUPANGISHA OFISI

MKATABA huu umeingiwa leo hii Tarehe 1st mwezi wa February 2024

KATI YA

ABDULAZIZ MUSSA

(Mwenye Ofisi)

NA

AL-JAWAD HOLDINGS(P)LIMITED

(Mpangaji)

UMEANDALIWA NA:

VANESSA SIKUBWABO NGENDABANKA

YWCA

P.O.BOX 11184, DAR ES SALAAM

Tel: +255712254671

Email: vanessasikubwabo@gmail.com

MKATABA WA KUPANGISHA OFISI

Mkataba huu umefanyika leo Tarehe 2nd mwezi wa **February** 2024.

BAINA YA

ABDULAZIZ MUSA wa Dar es Salaam Sinza (ambaye hapa atajulikana kama “Mwenye Ofisi”)

NA

AL-JAWAD HOLDINGS (P) LIMITED wa Dar es Salaam,Upanga (ambaye hapa atajulikana kama “Mpangaji”)

KWAMBA: Mpangaji amekubali kupanga ofisi iliyopo Wilaya ya ilala, upanga ,Plot 299 ,Maweni na Mwenye Ofisi kama ifuatavyo:

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA HAYA YAFUATAYO:-

1. Kwamba mwenye ofisi na mpangaji wamekubaliana, mpangaji atapanga kwa kipindi cha Miezi Mitatu na kuendelea kwa makubaliano.
2. Kwamba Mwenye ofisi na Mpangaji wamekubaliana kwamba mpangaji atalipa kodi ya miezi mitatu tarehe ya kuanza mkataba huu na ataendelea kulipa kila baada ya miezi mitatu.
3. Mwenye Ofisi amekubali mpangaji kupangisha Ofisi hiyo kwa fedha za Kitanzania Shilingi Laki Mbili (TZS 200,000) kwa kila mwezi.
4. Kwamba Mwenye Ofisi na Mpangaji wamekubaliana kwamba tarehe ya Mkataba huu Mpangaji atalipa kodi ya Miezi Mitatu ambyao ni Laki sita za kitanzania(600,000) .
5. Mpangaji atawajibika kuweka ofisi na mazingira yake katika hali ya usafi kipindi chote cha mkataba na kuhakikisha kuwa inakuwa katika hali ya kukalika muda wote atakao kuwa kwenye makataba, uharibifu wowote utakaofanywa na mapangaji au jamaa yake atawajibika kuufidia.
6. Mpangaji atalipa kodi ya umeme katika kipindi chote cha upangaji na huduma nyingine atakazokuwa anapata ambazo zinahitaji kulipiwa.

7. Mpangaji anapaswa kutoa taarifa ya maandishi kwa kipindi cha mwezi kabla kipindi cha mkataba kuisha kama atakuwa na nia ya kuendelea na mkataba.
8. Kipindi cha mkataba kikiisha kama mpangaji hakutoa taarifa za kuendeleza upangaji wake, itachukuliwa kuwa mpangaji hataki kuendeleza upangaji, hivyo mwenye nyumba atakuwa huru kupangisha mtu mwingine.
9. Mpangaji haruhisiwi kupangisha Ofisi kwa Mtu mwingine au kwa jamaa yake bila idhini ya wenye ofisi pia mpangaji Haruhisiwi kubadili matumizi ya upangaji bila idhini ya wenye ofisi.
10. Baada ya mkataba kuisha mpangaji atawajibika kukabidhi vitu vyote vinavyoambatana na ofisi na kukabidhi funguo na kuhakikisha vitu vyote viko salama na mpangaji na mwenye ofisi watakuwa huru kujadiri uendelezwaji wa mkataba mwingine.
11. KWAMBA endapo itatokea Mwenye Ofisi atavunja Masharti ya Makubaliano haya, Mpangaji anayo haki ya kuvunja mkataba huu na kurudushiwa pesa zote zilizobaki kwenye mkataba wake alizolipia na pia na fidia zozote alizongia.

MAKUBALIANO haya yametiwa sahihi leo tarehe 2nd mwezi February 2024 na wafuatao:

Imekubalika na kuwekwa sahihi hapa Arusha Mshono

Na **ABDULAZIZ MUSSA**

na kutolewa leo Tarehe 2nd mwezi February 2024

}



MWENYE OFISI

Imekubalika na kuwekwa sahihi hapa Dar es Salaam

Na **AL-JAWAD HOLDINGS (P) LIMITED**

na kutolewa leo

Tarehe 2nd mwezi February 2024

}



MPANGAJI

MBELE YANGU

Jina Kamili: Vanessa Sikubwabo Ngendabanka

Anwani: 11184 Dar Es Salaam

Wadhifa :Wakili

.....